Muhtasari kwa Lugha Nyepesi wa
Toleo la Hivi Karibuni la

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Tanzania

(Oktoba 2001)



Wizara ya Kilimo na Chakula
Wizara ya Ushirika na Masoko
Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo
Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa & Serikali za Mitaa

Februari 2005

Dibaji

Sekta ya Kilimo inaongoza kwa kuchangia kukua kwa uchumi wa Tanzania. Huchangia kwa zaidi ya nusu ya Pato la Taifa na mapato ya usafirishaji bidhaa nje. Sekta imekua kwa karibu asilimia 3 kila mwaka kwa miaka kumi iliyopita, lakini ukuaji huu umekuwa hautoshelezi ongezeko la watu au kupunguza umaskini. Zaidi ya asilimia 80 ya watu maskini nchini wanaishi vijijini ambapo maisha yao yanategemea kilimo. Hii ina maana ya kuwa ongezeko la kipato kinachotokana na kilimo ni muhimu katika kupunguza umaskini vijijini.

Dira ya Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo ni kuiwezesha sekta kuwa na sura ifuatayo ifikapo mwaka 2005:

- Kuwepo kwa kilimo cha kisasa
- Kilimo kuwa na mwelekeo wa biashara
- Kilimo kilicho na tija ya hali ya juu
- Kilimo kinacholeta faida
- Kilimo kinachohimiza matumizi endelevu ya raslimali
- Kilimo kinachochochea maendeleo ya sekta nyinginezo

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) ulichapishwa mwezi Oktoba 2001. Unalenga kuimarisha upataji faida wa shughuli za kilimo na biashara. Pamoja na mambo mengine mkakati utaongeza kipato cha mkulima na kupunguza umaskini vijijini.

Mkakati unahimiza mwelekeo wa kuwa mfumo wa uzalishaji unaozingatia soko ambapo sekta binafsi na ya umma zinashirikiana. Kuna aina tatu za mwelekeo ambazo zitasaidia utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo:

- Kulenga shabaha ya kuweka mazingira ya uwekezaji ambayo yatasaidia kukuza tija na faida katika kilimo.
- Kuimarisha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na pia kati ya wazalishaji mazao ya kilimo na wasindikaji.
- Kutekeleza mkakati kupitia Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo katika Wilaya (DADPs).

Mkakati huu ni matokeo ya utaratibu wa kupata ushauri mbalimbali. Ulibuniwa kwa kutumia Mtazamo Mpana wa Kisekta (SWAP) wa kuunda programu ya miaka mitano ya shughuli ambazo zinawiana na sera na programu nyingine za maendeleo. Mawazo katika ASDS yanapanuliwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP).

Lugha nyepesi imetumika kuelezea mkakati ili watu wengi zaidi waufahamu, kutoa maoni na kushiriki katika utekelezaji wake. Hali hii itajenga umiliki na uwajibikaji miongoni mwa wadau wengi katika utaratibu wa utelelezaji.

"Dira ya pamoja inaamsha hamu ya watu na kuleta shauku ambayo inaliinua taifa kutoka katika hali ya kawaida. Katika hatua hiyo, inafundisha ujasiri na azma ya kuleta changamoto katika ngazi ya mtu binafsi, jumuiya na taifa".

Dira ya Maendeleo Tanzania 2025

Yaliyomo

Utangulizi 1

Maswali na Majibu 1

Ni kitu gani kipya na tofauti kuhusu Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS)? 2

Ni masuala gani muhimu sana katika ASDS? 4
1. Kuimarisha muundo wa kitaasisi. 5
2. Kujenga mazingira mazuri kwa shughuli za biashara.. 6
3. Wajibu wa sekta ya umma na binafsi katika kuboresha huduma za msaada 7
4. Kuimarisha ufanisi wa masoko kwa pembejeo na mazao 8
5. Kuhusisha mipango kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika sekta nyingine. 9

Nani walihusishwa kuunda Mkakati? 10

ASDS itatekelezwa kwa namna gani? 12

Ni malengo gani yamewekwa na ni hatua gani zinazofuata? 13

Itagharimu kiasi gani kutekeleza ASDS? 15

Uendeshaji wa ASDS utakavyoratibiwa na kufanyiwa tathmini yake. 17

Mchoro wa Menejimenti ya ASDS/ASDP 18

Faharasa: Maana za maneno yaliyotumika katika kitabu hiki **19**

Vifupisho **23**

Kiambatisho 1 – ASDP – Programu ndogo tatu **24**
Utekelezaji wa sekta ya kilimo katika ngazi ya wilaya na ugani 24
Sekta ya kilimo ngazi ya taifa 24
Masuala yanayogusa sekta nyingine katika ngazi ya taifa 24

Shukrani **25**

Utangulizi

Toleo hili la Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) kwa kugha nyepesi linaeleza hoja muhimu kwa kujibu maswali saba yanayoulizwa mara kwa mara. Haya hayahusiani tu na maudhui bali pia na utaratibu ambao ulitumika katika kuunda Mkakati wenyewe.

Faharasa na orodha ya vifupisho vimetolewa mwishoni mwa kitabu. Wasomaji ambao hawayafahamu maneno ambayo yanatumika katika sekta ya kilimo na maendeleo watasaidiwa sana na orodha hiyo.

Maswali na Majibu

Wazo kuu katika ASDS na utaratibu wake umeelezwa kwa ufupi katika orodha ya maswali na majibu ifuatayo:

1. Ni kitu gani kipya na tofauti kuhusu ASDS?
2. Ni masuala gani muhimu sana katika ASDS?
3. Nani walihusishwa katika kuunda Mkakati?
4. ASDS itatekelezwa kwa namna gani?
5. Ni malengo gani yamewekwa na ni hatua gani zinazofuata?
6. Itagharimu kiasi gani kutekeleza ASDS?
7. Utekelezaji wa ASDS utaratibiwa na kutathminiwa namna gani?

Ni kitu gani kipya na tofauti kuhusu ASDS?

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) una mahusiano ya wazi na muhimu kwa mageuzi mengine ya uchumi makubwa na marekebisho ya kimuundo nchini, yanayoongozwa na Dira ya Maendeleo Tanzania 2025 na Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRS). Kwa hiyo, kipaumbele ni kupunguza umaskini. Muhtasari wa uhusiano wa PRS na Dira ya Maendeleo 2025 umetolewa katika kielelezo hapa chini.



Malengo ya muda wa kati ya ASDS yanayotokana na Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Malengo ya muda mrefu ya ASDS yanatokana na Dira ya Maendeleo 2025. Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Dira 2025 unabaini umuhimu wa kilimo katika kupunguza umaskini na kuinua hali ya ustawi wa Watanzania.

Katika kusimamia mageuzi yanayoendelea, serikali ina wajibu ufuatao:
(a) Kubuni sera
(b) Kurekebisha mfumo wa utendaji
(c) Kusimamia na kutoa huduma za umma pamoja na kuweka mazingira yanayohimiza maendeleo. Aidha wajibu mwingine ni kuweka mfumo wa ulinzi kwa jamii zilizo na hatari zaidi ya kuathirika.

Kutokana na majukumu haya, serikali haitakuwa mwekezaji mkubwa sehemu ambazo sekta binafsi inaweza kufanya hivyo. Mtazamo huu umebainishwa pia katika Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

Maudhui ya ASDS yanatambua mikakati na sera mahususi mbalimbali zilizopo. ASDS inabaini kama ni sehemu ya Mkakati wa Maendeleo Vijijini unaojumuisha kilimo, shughuli zisizo za kilimo, huduma za kijamii, kiuchumi na miundo mbinu. Pia ASDS imezingatia mikakati mingine iliyopo, kuhusu sera na programu za mageuzi. Tukumbuke kuwa mkakati huu ni kipengele cha kisekta cha Mkakati wa Maendeleo Vijijini.

ASDS inalenga kujenga mazingira mazuri ambayo yataboresha upataji faida katika kilimo kwa kuwanufaisha wakulima kwa kujikimu na kwa biashara. Moja ya mawazo makuu ni kubadilisha kilimo cha kujikimu kuwa katika kilimo kinachofaa zaidi na chenye faida kibiashara. Hii itaongeza kipato cha mkulima na kupunguza umaskini vijijini.

Wazo jingine kuu ni kuwa utaratibu wa ushiriki na ushauri utasaidia kuhakikisha kuwa sekta za umma na binafsi zinashirikiana katika uratibu na utekelezaji. Serikali italenga katika kuunda sera na kubuni miundo ya udhibiti ambayo inahamasisha sekta binafsi kuwa na wajibu muhimu katika kujenga utajiri, viwanda binafsi vya huduma za kilimo, vya moja kwa moja au kwa ushirikiano na wafanyabiashara wadogo. Viwanda binafsi vinavyohusika na mazao ya kilimo vitahusishwa zaidi na uzalishaji wa awali na pia usambazaji wa pembejeo, masoko na usindikaji bidhaa za kilimo kuanzia ngazi ya kijiji mpaka taifa. Kwa njia hii sekta

"Kilimo cha Tanzania, kama ilivyo kwa uchumi wote, kipo katika mpito kutoka katika 'udhibiti' kwenda katika mfumo wa uzalishaji "unaozingatia soko".

(ASDS (2001) uk 1)

binafsi itakuwa inaongoza katika kuboresha mkakati huu.

ASDS ni matokeo ya ushauri mbalimbali na unaweka muundo mpana kwa programu ya shughuli ya miaka mitano. Unasaidiwa na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) ambayo inatoa mwongozo kwa ajili ya kuunda programu endelevu ya miaka mitatu ambayo itataarifu utayarishaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya katika ngazi ya chini.

Mbinu za ushirikishwaji zilisaidia kuzingatia mtazamo mpana wa kisekta (angalia kisanduku). Pia utaratibu huu ulisaidia kuzingatia yafuatayo:-

- Uwiano wa sera
- Kuwajibika kwa mihadi ya wafadhili
- Uhusiano katika wizara na baina ya sekta kwa ajili ya uhusianishaji na uratibu katika ngazi za juu
- Kwamba wadau nchini wanakuwa mstari wa mbele

ASDS inatumia Mtazamo Mpana wa Kisekta (SWAP) - ambao unahusisha kuzingatia ushiriki, utaratibu wa wadau wengi kujenga (a) uelewa wa jumla wa matatizo yanayoikabili sekta na kisha (b) mwitiko unaoeleweka na ulioratibiwa kwa matatizo hayo.

Wadau mbalimbali wanaona faida endapo serikali itakuwa mstari wa mbele katika kutoa mwongozo wa utekelezaji, uratibu wa wafadhili, mipango na upangaji bajeti unaoeleweka, taratibu za kawaida za utekelezaji, kupunguza fedha za matumizi, mkazo katika utoaji fedha unaozingatia utendaji, ongezeko la mwelekeo katika rasilimali, na kwa ujumla kuwezesha mchakato wa ugawaji madaraka.

Itambulike kwamba mkakati unatoa wito wa ufuatiliaji na tathmini yenye utaratibu wa mara kwa mara katika ngazi zote. Hii inatumika kama mbinu ya kupata marejesho ya maoni katika utaratibu unaondelea wa ushiriki na mashauriano.

Kwa hiyo, ni kitu gani kipya na tofauti kuhusu mkakati huu? Mawazo makuu pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa vimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo.

Wazo kuu	**Hatua**
Kulenga katika mifumo ya uzalishaji kilimo yenye ufanisi na upataji faida	• Kuhamasisha upanuzi wa bidhaa ili kupanua masoko ya ndani na usafirishaji bidhaa nje. • Kuwahamasisha wakulima kuzalisha kufuatana na mahitaji ya soko. • Kuongeza miradi ya uzalishaji bidhaa za kilimo ikilenga katika kupunguza hasara na uharibifu baada ya mavuno.
Kukuza ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma, na pia kati ya biashara ya kilimo na wakulima wa mkataba	• Kuhimiza ugharimiaji zaidi wa sekta binafsi katika msaada wahuduma. • Kuhamasisha ushirikiano kati ya watengenezaji na wazalishaji wadogo ili kuhakikisha malighafi za kudumu kwa watengenezaji na upatikanaji wa pembejeo, teknolojia na masoko kwa wazalishaji wadogo.
Kutekeleza na kufuatilia ASDS kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya kwa kutumia ushiriki na mashauriano	• Kuhamasisha mawasiliano mazuri kati ya wadau wa ngazi mbalimbali na kati ya ngazi. • Kutumia ASDS na ASDP kama miongozo ya kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. • Kuwahamasisha wadau wote kukabiliana na changamoto ya kufanya kazi katika mashauriano shirikishi.

Ni masuala gani muhimu sana katika ASDS?

Mkakati huu unaainisha masuala matano ambayo ni muhimu kuleta maendeleo ya sekta ya kilimo nchini Tanzania.

1. Kuimarisha utendaji wa taasisi katika kusimamia maendeleo ya kilimo.
2. Kuweka mazingira ya kibiashara ambayo yanavutia ushiriki wa sekta binafsi.
3. Kubaini majukumu ya sekta ya umma na ile ya binafsi ili huduma kwa sekta ya kilimo ziwe bora.
4. Kuimarisha ufanisi wa masoko kwa pembejeo na bidhaa za kilimo ili kukuza kipato na kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara.
5. Kuwezesha mipango ya maendeleo ya kilimo kuwemo katika sekta nyinginezo.

Mbali ya masuala haya kuainishwa kuwa ni muhimu, yanashabihi jukumu la serikali la kurekebisha mfumo wa utendaji na kuweka mazingira bora kwa watekelezaji. Aidha masuala haya yanatoa fursa kwa serikali za mitaa na jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza ASDS.

Jedwali lifuatalo linaonyesha maeneo makuu matano na jinsi yanavyohusiana katika lengo, madhumuni na shabaha za kimkakati za ASDS.

Lengo	•	Kuchangia kwa ongezeko katika (a) ukuaji mzima wa uchumi, (b) kipato cha taifa na kaya, na (c) mapato ya usafirishaji bidhaa nje
Madhumuni	•	Kuchochea na kusaidia ukuaji wa sekta ya kilimo na hivyo kupunguza umaskini wa vijijini
Shabaha kimkakati	•	Kujenga mazingira mazuri yanayofaa na yatakayoboresha tija na upataji faida wa sekta ya kilimo
	•	Kuongeza kipato cha mkulima ili kupunguza umaskini vijijini na kuhakikisha kuwepo kwa uhakika wa chakula ngazi ya kaya
Maeneo ya Mkakati	1	Kuimarisha muundo wa kitaasisi
	2	Kujenga mazingira mazuri yanayofaa kwa shughuli za biashara
	3	Kuelekeza majukumu ya sekta ya umma na binafsi katika kuendeleza huduma zitakazotolewa
	4	Kuimarisha ufanisi wa soko kwa pembejeo na mazao
	5	Kuhusisha mipango ya maendeleo ya kilimo katika sekta nyingine

Katika kurasa zinazofuata tutaangalia kwa kina yanayohusishwa katika kila moja ya maeneo matano ya kimkakati.

1. Kuimarisha muundo wa kitaasisi

Muundo huu wa kitaasisi una watu mbalimbali wanaofanya mambo tofauti ama wao wenyewe au kama sehemu ya mashirika ya serikali au ya sekta binafsi au biashara. Mfumo utakuwa na ufanisi zaidi kama watu wote hawa wanaweza (a) kujadiliana na kukubaliana katika malengo na shabaha za pamoja na (b) kuboresha maarifa na ujuzi wao kuhusu mawasiliano shirikishi na kuhusu biashara changamani ya sera, mipango ya programu na mradi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini.

Eneo la Mkakati 1	Kuimarisha muundo wa kitaasisi	
Matokeo	1.1	Kuanzisha muundo wa uratibu wa ASDS
	1.2	Uwezo wa Wizara kiongozi kuimarishwa
	1.3	Uwezo wa Sekretarieti za Mikoa kuimarishwa
	1.4	Uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarishwa
	1.5	Vyama vya wakulima kukuzwa
	1.6	Uwezo wa sekta binafsi kuboreshwa
	1.7	Uwezo wa vyama vya kiraia kuboreshwa
	1.8	Kuboresha utangazaji wa masuala ya sekta ya kilimo katika vyombo vya habari
	1.9	Kuwepo kwa huduma inayofaa ya Upimaji wa Ardhi

Shughuli zilizo nyingi katika eneo hili la mkakati zinahusisha kubainisha majukumu, shughuli za uratibu na kujenga uwezo.

2. Kujenga mazingira mazuri yanayofaa kwa shughuli za biashara

Hii inahusisha kujenga mazingira ya uchumi mkubwa ambayo yanavutia uwekezaji binafsi - masuala yanayohusisha vitu kama kodi, ada, ushuru, ushuru wa forodha, viwango vya kubadili fedha, viwango vya kukopa benki n.k. Pia inahusu kupitia upya, kuwianisha na kutekeleza aina nyingine za sheria na kanuni ambazo zinaathiri sekta ya kilimo ama moja kwa moja au siyo moja kwa moja – kwa mfano, umiliki wa ardhi ni tatizo kubwa katika maeneo mengi nchini.

Eneo la Mkakati 2	Kujenga mazingira mazuri kwa shughuli za biashara	
Matokeo	2.1	Kudumisha uthabiti wa uchumi mkubwa
	2.2	Sheria za sekta ya kilimo kupitiwa upya, kuwianishwa na kutangazwa
	2.3	Sheria za sekta zinazoshirikiana kupitiwa upya, kuwianishwa na kutangazwa
	2.4	Kutolewa uwezo wa kisheria kwa wadau watakaohusishwa katika usimamizi wa Bodi ya Bidhaa
	2.5	Biashara ya mipakani itahalalishwa na kukuzwa
	2.6	Sera ya uhakika wa chakula itaundwa na kutekelezwa
	2.7	Taratibu za upatikanaji wa ardhi kisheria kuwianishwa
	2.8	Upimaji wa ardhi na uwekaji mipaka kwa kanda za uwekezaji wa kilimo kufanyika

Shughuli zilizo nyingi katika eneo hili la mkakati zinahusu kupitia na kuwianisha sheria, na kuhusika ipasavyo na biashara ya mipakani, uhakika wa chakula na masuala ya matumizi ya ardhi.



3. Wajibu wa sekta ya umma na binafsi katika kuboresha huduma za msaada

Huduma kwa sekta ya kilimo zinajumuisha utafiti, ugani, mafunzo na pia taarifa, usimamizi wa kanuni, huduma za kisheria na fedha. Ni muhimu kwamba huduma hizi zipatikane kwa wingi na kwa ubora zaidi. Pia huduma zinapaswa kutolewa kwa msingi wa kumjali mteja kulingana na mahitaji. Wazo ni kujenga ushirikiano wa kuchangia gharama ili kupanua msingi wa mashirika ambayo yanaweza kutoa huduma hizi.

Eneo la Mkakati 3	Wajibu wa sekta ya umma na binafsi katika kuboresha huduma za misaada	
Matokeo	3.1.	Kufuata utafiti wa kilimo unaozingatia mteja na wa ushirikiano
	3.2	Kufuata mahitaji yenye uelekeo wa kilimo cha ugani
	3.3.	Kuzingatia mahitaji ya mafunzo yenye uelekeo wa kilimo
	3.4	Kuimarisha huduma za kisheria na kanuni
	3.5	Kuimarisha huduma za afya ya wanyama na ulinzi wa mazao
	3.6	Kuboresha usimamizi wa eneo la malisho
	3.7	Kuboresha usimamizi na matumizi ya ardhi na rasilimali za maji
	3.8	Kuimarisha kilimo cha mashine
	3.9	Kutumika kwa mfumo wa taarifa za kilimo unaoeleweka
	3.10	Kuimarisha na kukuza asasi ndogo za fedha za wananchi
	3.11	Kuanzisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya fedha za uwekezaji

Kuna hatua nyingi za kina katika eneo hili la mkakati. Nyingi zinahusisha kuanzisha njia mpya na shirikishi zaidi za kutoa huduma – katika hali iliyoratibiwa, fanisi na yenye gharama nafuu.

4. Kuimarisha ufanisi wa masoko kwa pembejeo na bidhaa

Lengo hapa ni kuongeza vipato vya kilimo kwa kipindi cha muda mfupi na kuongeza faida kwa kilimo cha biashara katika kipindi cha muda mfupi mpaka muda mrefu. Matokeo ya kufanikisha mkakati huu yana viwango mbalimbali vilivyoingiliana ambavyo vinajumuisha kujenga miundombinu ya vijijini, kukuza ushirikiano kati ya wakulima wadogo na wafanyabiashara wa kilimo, kuboresha mifumo ya habari za masoko, kuboresha uzalishaji bidhaa za kilimo na ujengaji viwanda vijijini na kubuni taratibu za motisha.

Eneo la Mkakati 4	**Kuimarisha ufanisi wa masoko kwa pembejeo na bidhaa**	
Matokeo	4.1	Kuanzishwa kwa Kitengo Binafsi cha Msaada wa Sekta ya Viwanda vya Huduma za Kilimo
	4.2	Kukuza usindikaji bidhaa za kilimo na ujenzi wa viwanda vijijini
	4.3	Kuongeza upatikanaji wa pembejeo maeneo ya vijijini
	4.4	Kuimarisha ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko
	4.5	Kuboresha miundombinu ya vijijini kwa masoko ya pembejeo na mazao ya kilimo
	4.6	Kukuza ushirikiano kati ya wakulima wadogo na biashara ya kilimo
	4.7	Kuanzisha taratibu za motisha kwa uwekezaji wa kilimo

Shughuli kwa ajili ya eneo hili la mkakati zinashauri kuwa shughuli nyingi zilizopendekezwa tayari zipo lakini hazifanyi kazi ipasavyo katika sehemu nyingi. Kwa hiyo, miongoni mwa mambo ya kufanikisha hatua hizi ni kuchunguza, kuhakiki, kuanzisha, kukarabati, kukuza, kubuni na kuendeleza.



5. Kuhusisha mipango kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika sekta nyingine

Maendeleo ya kilimo na maisha ya vijijini vinaathiriwa sana na masuala ambayo yako nje ya udhibiti wa moja kwa moja wa Wizara Kiongozi kwa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS). Hii inatoa wito kwa mashauriano ya sekta zinazoingiliana kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi za chini.

Eneo la Mkakati 5	Kuhusisha mipango kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika sekta nyingine	
Matokeo	5.1.	Kuboresha miundombinu ya vijijini chini ya Mkakati wa Maendeleo Vijijini
	5.2	Kuboresha uwekaji wa umeme na mawasiliano vijijini
	5.3	Kupunguza athari za VVU/UKIMWI
	5.4	Masuala ya jinsia kuhusishwa katika mipango ya maendeleo ya kilimo
	5.5	Kuwapa fursa vijana
	5.6	Kuimarisha usimamizi wa mazingira

Shughuli zilizopendekezwa ni mahususi kwa masuala ambayo yameshabainishwa; haya ni pamoja na miundombinu ya vijijini (hasa uwekaji umeme na mawasiliano), VVU/UKIMWI, jinsia, vijana na mazingira.



Nani walihusishwa katika kuunda mkakati?

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) unapaswa kuzingatia na kwenda pamoja na mikakati mingine ya serikali, sera na programu za marekebisho. ASDS imetokana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 na kuzingatia:

(a) Mkakati wa Maendeleo Vijijini, Mkakati wa Kupunguza Umaskini;
(b) Sera za Mazingira, Jinsia, Ardhi, Vyombo vya Fedha na Maji; na
(c) Programu za Marekebisho ya Uchumi Mkubwa, Serikali za Mitaa na Sekta ya Umma.

Baadhi ya hizo ni matokeo ya michakato mingi ya mashauriano.

Kamati ya Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
- Wizara ya Kilimo na Chakula
- Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji
- Wizara ya Fedha
- Ofisi ya Waziri Mkuu
- Ofisi ya Rais – Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa
- Wabia wa Serikali katika Maendeleo

Kati ya mwaka 1995 na 1997 kulikuwa na mashauriano kuhusu Sera ya Kilimo na Mifugo na Sera ya Maendeleo ya Ushirika. Kati ya mwaka 1998 na 2000 kulikuwa na tafiti na mashauriano vilivyolenga katika kupitia upya utendaji wa sekta na kupendekeza shughuli ambazo zitawezesha upataji faida. Shughuli hizi ni pamoja na mashauriano katika Mradi wa Usimamizi wa Sekta ya Kilimo na Mradi wa Kilimo wa Huduma za Ugani wa Taifa. Mwezi Septemba 1999, Waziri Mkuu aliteua Kamati Maalumu ya Ushauri katika Kilimo na mwezi Aprili 2000, Rais aliteua Kikundi Maalumu katika Ushirika. Vikundi vyote viwili viliomba ushauri nchi nzima na matokeo yake yameunda ASDS.

Tafiti na ripoti mbalimbali pia zimeuelezea mkakati. Tafiti tatu muhimu ni:
- Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (1999) *Taarifa ya Kamati Maalumu ya Ushauri kuhusu Maendeleo ya Kilimo nchini Tanzania, masuala na mapendekezo.*
- Wizara ya Kilimo na Ushirika & Benki ya Dunia (Februari 2000) *Kilimo nchini Tanzania: Utendaji na Mikakati ya Ukuaji Endelevu.*
- Benki ya Dunia na IFPRI (2000) *Kilimo nchini Tanzania 1986: Mfuasi au Kiongozi wa Ukuaji.*

Ripoti mbili zilizotayarishwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo mapema mwaka 2001 pia zilihusisha mashauriano. Ripoti hizi zilithibitishwa kufaa sehemu za ASDS zinazohusu sekta ndogo ya mifugo.

Warsha mbili za wadau zilifanyika Bagamoyo mwaka 2002. Warsha ya kwanza ilifanyika kuanzia Mei 29 hadi Juni 1 na ilihusisha wadau 50 ambao walisaidia kutayarisha waraka wa mkakati. Warsha ya pili ilikuwa Septemba 11-12 na ilihusisha wadau 59 ambao waliupitia mkakati. Wadau katika mikutano hii walitoka katika Wizara mbalimbali, mashirika ya umma, asasi za elimu, mashirika wafadhili na mashirika ya kimataifa.

Uwezekano wa vikwazo kwa mkakati kama ilivyobainishwa wakati wa mashauriano mwaka 2000:

- Asasi dhaifu na zisizofaa
- Msingi hafifu wa mtaji na ukosefu wa huduma za vyombo vya fedha
- Upungufu wa huduma za msaada
- Miundo mbinu duni vijijini
- Sekta haikupewa kipaumbele inachostahili katika mipango ya jumla na ugawaji wa fedha

Mwezi Septemba 2000 rasimu ya ASDS iliwasilishwa Serikalini na iliamuliwa waraka uboreshwe kwa mashauriano zaidi, hasa kwa wadau wa ngazi ya chini katika maeneo ya vijijini. Hii ilisababisha kuwepo na warsha nne za siku mbili mbili mwishoni mwa mwezi Machi na mwanzoni mwa Aprili 2001. Warsha hizo zilifanyika Mwanza, Njombe, Bagamoyo na Dodoma.

Kati ya washiriki 195 wa warsha hizo, 78 walikuwa wanawake na 103 walikuwa wakulima na wawakilishi wa wakulima. Utaratibu wa wawakilishi umeonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Mwakilishi	**Asilimia**
Wakulima wadogo na wafugaji	35
Wakulima wa kati na wakubwa	5
Wawakilishi wa vyama vya wakulima	13
Viongozi wa Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya	17
Madiwani wa Serikali za Mitaa, AZISE na wanaotoa huduma ngazi ya chini	13
Maofisa wa Serikali kuu	17

ASDS ilirekebishwa kufuatia maoni kutoka katika Warsha nne za Kanda. Toleo lililofanyiwa marekebisho liliwasilishwa katika awamu nyingine ya warsha ya wadau tarehe 7-8 Juni 2001, ambayo pia ilisababisha baadhi ya marekebisho. Toleo la mwisho la ASDS liliwasilishwa katika warsha ya wizara na wawakilishi wa wabia wa maendeleo tarehe 27 Septemba 2001 na kuchapishwa Oktoba 2001.

Mada za kushughulikiwa kufuatia mashauriano ya 2001:
- Marekebisho ya taasisi na sheria
- Mazingira ya kiutawala na kisheria
- Uthabiti wa uchumi mkubwa
- Uwekezaji na fedha
- Miundombinu vijijini
- Soko la pembejeo na mazao
- Usimamizi wa mazingira asili na rasilimali
- Uwezo na uwezeshaji wa wananchi
- Huduma za msaada

Kumbuka kuwa utaratibu wa mashauriano haujaisha. Mkakati wa kwanza wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo una kipindi cha miaka mitano. Mkakati huu utapitiwa tena kufuatana na maoni ya watu ambao wanahusishwa katika kuutekeleza. Ni mkakati hai. Umebuniwa ili kila mtu aweze kuchangia jinsi unavyokua.

Muundo wa utawala (angalia ukurasa wa 19) umeundwa kuhamasisha demokrasia na ushiriki wa wananchi ambao unaunda sehemu muhimu ya Dira ya Maendeleo Tanzania ya 2025 (Angalia kisanduku).

Dira ya Maendeleo Tanzania 2025 inatambua kuwa ili kukuza demokrasia na ushiriki wa wananchi, pamoja na mambo mengine, kuna haja ya:
- Kuruhusu wajibu mkubwa kwa watendaji wa chini kumiliki na kuleta maendeleo yao. Wananchi wanajua matatizo yao vizuri na wana nafasi nzuri ya kuamua wanachokitaka, mafanikio yanayowezekana na jinsi ya kupatikana vizuri.
- Utawala wa kisiasa na wajibu na majukumu ya muundo na utaratibu wa hazina ya serikali hauna budi kuzingatia misingi ya kanuni za uwajibikaji wa watu binafsi, kaya, jumuiya na serikali za mitaa kufikia Dira ya jumla

DMT 2025

ASDS itaendeshwa namna gani?

Inasaidia kufikiria mipango kuwa na ngazi kuu mbili. Ngazi ya kwanza ni kuwa na mipango ya kimkakati ambayo kwa jumla inahusika na kinachotakiwa kufanyika. Ngazi ya pili ni upangaji programu. Hii inafuatia ngazi ya kwanza na inahusisha kuamua nani atafanya nini ifikapo lini (na itagharimu kiasi gani na itagharimiwaje). Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) unaelezea ngazi ya kwanza na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) inaelezea ngazi ya pili. Kumbuka kwamba ASDP inapanga shughuli za ASDS ili iwe rahisi kusimamia utekelezaji wake. (Angalia kiambatisho cha 1).

Maudhui ya ASDS na ASDP yaliamuliwa baada ya mashauriano ya watu wengi ambayo yanaendelea. Vyote viwili, Mkakati na Programu vitarekebishwa kutokana na maoni ya watu ambao wanajaribu kuitumia.

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Mipango ya Kimkakati	**Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Mipango ya Programu**
ASDS inatoa maelezo ya kina na muundo wa kufanikisha malengo na shabaha za sekta ya kilimo.	ASDP inataja kwa kina jinsi mkakati utakavyotekelezwa.
Muundo wa muda wa miaka mitano	Muundo wa muda endelevu wa miaka mitatu
ASDS ina maeneo 5 ya mkakati yaliyogawanywa katika matokeo 41 na shughuli 142.	ASDP ina programu ndogo 3 zenye vipengele 10, vipengele vidogo 61 vilivyopendekezwa, na uwezekano wa shughuli 111.

Kumbuka kwamba ASDS na ASDP ni miongozo si mipango. Haziweki orodha ya kina ya mambo yanayopaswa kufanywa sehemu zote za nchi. Zinatoa muundo wa utaratibu ambao jumuiya na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatumia kuamua ni kitu gani kijumuishwe katika Mipango yao ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

Kumbuka kwamba makala kuu ya ASDP ilitengenezwa kwa mashauriano kati ya kamati za uratibu ndani ya Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazofanya kazi kupitia Sekretarieti za Mkoa.

> Kupitia utaratibu huu jumuiya za wenyeji zitakuwa na uwezo wa kubadilika katika kutekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Utekelezaji huu shirikishi katika ngazi ya jumuiya utahakikisha uendelevu na kuwaamini watu wa vijijini na hatima yao.
>
> Kwa Wizara zinazoongoza, utaratibu huu unatoa changamoto kwa kuhitaji njia mpya ya kufanya kazi na taratibu mpya na zinazofaa za mawasiliano na jumuiya za wenyeji.
>
> (ASDS, 2001, uk. 23)

Programu inaweza kutumiwa katika ngazi ya Wilaya kusaidia kuorodhesha na kuweka vipaumbele vya shughuli kwa eneo hilo mahususi. Kisha kila Wilaya itakuwa na programu yake ambayo inafaa kwa mazingira na mahitaji yake.

Ni malengo gani yamewekwa na hatua gani zinazofuata?

Lengo hutoa mwelekeo wa kitu unachotaka kufanya (linasaidia kusema utafanya kwa kiasi gani ifikapo tarehe ngapi). Ni vigumu kuweka malengo halisi kwa sekta ya kilimo kwa sababu kuna mambo mengi sana yanayoweza kubadilika. Lakini bado ni muhimu kuyaweka kwa sababu yanatoa mwelekeo wazi. Yanaweza kupitiwa upya jinsi taarifa mpya zinavyotokea au jinsi hali inavyobadilika.

Malengo yanapaswa kuoanishwa na shabaha kimkakati. Kwa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS) haya ni

(a) Kujenga mazingira wezeshi na mazuri ambayo yanaboresha tija na upataji faida wa sekta ya kilimo na

(b) Kuongeza pato la mkulima na ili kupunguza umaskini vijijini na kuhakikisha kuna uhakika wa chakula kwa kaya.

Malengo makuu ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini (kama yalivyowekwa 2000)

- Kupunguza uwiano wa idadi ya watu walio chini ya mstari wa umaskini kutoka 48% mwaka 2000 hadi 42% mwaka 2003 na 24% ifikapo 2010.
- Kupunguza uwiano wa idadi ya watu vijijini walio chini ya mstari wa umaskini kutoka 57% mwaka 2000 hadi 49.5% mwaka 2003 na 29% mwaka 2010.
- Kupunguza uwiano wa chakula kwa maskini kutoka 27% mwaka 2000 hadi 23.5% mwaka 2003 na 14% mwaka 2010.

Mkakati wa Kupunguza Umaskini na ripoti zake mbalimbali za maendeleo zimeweka na kupitia upya malengo ya kupunguza umaskini na kilimo (angalia visanduku) lakini hili lilikuwa kabla ya uchambuzi kamili wa sekta kufanyika. Matatizo makuu matatu yamejitokeza katika kuongeza tija ya kilimo katika kipindi cha miaka mitano ya muundo wa ASDS –

- Sehemu kubwa ya kilimo inategemea teknolojia ya jembe la mkono na kuna uhaba wa nguvu kazi maeneo ya vijijini. Itachukua muda kubadili mifumo ya ukulima na kuanzisha utumiaji mashine katika kipimo kinachofaa.
- Programu za Marekebisho ya Serikali za Mitaa na Utumishi wa Umma bado ziko katika hatua za mwanzo. Itachukua miaka kadhaa ili kufanya miundo hii ifanye kazi ipasavyo na hivyo kutoa huduma bora kwa ajili ya sekta.
- Michango inayotokana na usafirishaji bidhaa nje kwa ajili ya soko la dunia kwa kiasi kikubwa haitabiriki.

Lengo la ukuaji kwa sekta ya kilimo katika Ripoti ya Maendeleo ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini ya 2000/2001

- Kuongeza ukuaji wa mwaka wa pato ghafi la ndani la kilimo kutoka 3.6% hadi 5% ifikapo 2003 na hadi 6% ifikapo 2005.
- Kuongeza kiwango halisi cha ukuaji wa mwaka wa kipengele cha mifugo kutoka 2.7% hadi 5% ifikapo 2005.
- Kuongeza kiwango halisi cha ukuaji wa mwaka wa usafirishaji mazao nje kutoka 6.7% hadi 9% ifikapo 2005.



Kutokana na hayo hapo juu, mpango ulio wazi zaidi kwa ajili ya Sekta ya Kilimo ni kuwa na kiwango cha wastani cha ukuaji kwa mwaka cha asilimia 5 kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia 2005 hadi 2007. Mpango huu ukizingatiwa utakuza ajira vijijini na kusaidia sana kufikia malengo ya kupunguza umaskini.

Hatua inayofuata inahusisha miaka mitano ya ASDS kwa kutumia programu endelevu ya miaka mitatu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Faida za programu hizi zitategemea:

- Upatikanaji wa fedha
- Uwezo wa Wizara, Programu na Mamlaka za Serikali za Mitaa wa kusambaza na kutumia fedha ipasavyo
- Kipaumbele kilichotolewa katika shughuli mbalimbali na matokeo katika ngazi kuu na wakati wa kuunda programu za kiwilaya
- Njia ambazo shughuli zimepangwa.

Malengo na viashiria vilivyowianishwa

Tunahitaji idadi ya malengo na viashiria vilivyowianishwa ili tuweze kusema kama tunaelekea kunakofaa. Ni vizuri kufikiria aina tatu:

Malengo na Viashiria kuhusu utaratibu wa kutekeleza programu na mkakati vinatusaidia kupima kiasi ambacho wadau wanafanya mambo katika njia mbalimbali. Hii itajumuisha kiwango ambapo:

- Miradi ya kawaida toka ngazi ya taifa inabadilishwa na shguhuli zinazozingatia utoaji maamuzi katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Jumuiya unazingatiwa.
- Serikali kuu inatoa kiasi sahihi cha fedha kwa muda muafaka kwa Wilaya na vijijini.

Malengo na Viashiria vya kati vinatusaidia kupima kiwango cha maendeleo kuelekea malengo ya muda mrefu. Hii itajumuisha mambo kama

- Kuongeza viwango vya uwekezaji wa sekta binafsi
- Utoaji wa huduma mbalimbali zenye ubora.
- Kiwango cha hatua na jamii zenye fursa.

Malengo na Viashiria vinavyoonyesha mabadiliko yanayozingatia kiwango cha juu cha malengo ya maendeleo. Hii itaonyesha jinsi sekta ya kilimo inavyochangia katika kuendeleza uchumi wa taifa na kupunguza umaskini. (angalia visanduku vilivyotangulia kwa mifano).

Itagharimu kiasi gani kutekeleza ASDS?

ASDS itatekelezwa kupitia ASDP ambayo ina programu ndogo tatu (angalia kiambatisho cha 1). Ni vigumu kuwa sahihi kuhusu gharama, lakini makadirio ya sasa ni kuwa kiasi cha Tsh. bilioni 600 kitahitajika katika miaka mitano ijayo. Ugharimiaji utatoka katika vyanzo vikuu vitano vilivyoonyeshwa katika kisanduku. Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2003/04 kwa ajili ya Wizara Kiongozi ya Sekta ya Kilimo ni Tsh. bilioni 65. Kati ya hizo, Tsh. bilioni 38 ni kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Tsh. bilioni 26 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo. Kumbuka kwamba asilimia 90 ya Bajeti ya Maendeleo inatokana na michango ya wafadhili na wafadhili hao wanatoa kiasi cha Tsh. bilioni 17 nyingine nje ya Bajeti.

Matumizi katika sekta ya kilimo yataongezeka kama ASDS na ASDP zitahitaji kufanikiwa, huenda kiasi cha asilimia 20 kila mwaka. Hatua hii imeshaanza. Hata hivyo, kumbuka kwamba kuweka fedha katika sekta ya umma hakuwezi kuleta mafanikio makubwa isipokuwa kama zitatumika vizuri na kwa busara. Kwa hiyo, sehemu ya uwekezaji itatumika kuhakikisha kuwa ujuzi wa watumishi wa umma unaboreshwa na kuwa wadau wote husika wanafahamu kile kilichopangwa.

Vyanzo vya ugharimiaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo:

- Bajeti ya serikali
- Wafadhili na Asasi za Fedha za Kimataifa (ruzuku au mikopo inayotolewa ama moja kwa moja katika miradi, au kupitia Bajeti ya Serikali)
- Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa
- Fedha za vijiji na jumuiya (ikiwa ni pamoja na programu na miradi ya Asasi zisizo za Serikali na Vyama vya Kiraia)
- Msaada wa sekta binafsi pia unaweza kupatikana, lakini hii haionekani kama sehemu ya ASDP. Itajumuisha rasilimali zinazotolewa na wakulima, wafanyabiashara, wasindikaji bidhaa za kilimo na wadau wengine. ASDP itahamasisha na kurekodi aina hii ya uwekezaji kwenye sekta.

Majedwali mawili katika kurasa mbili zinazofuata yanaonyesha utabiri unaozingatia utekelezaji wa programu ndogo tatu za ASDP. Katika utabiri huu lengo ni kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya fedha zinatengwa kwa ajili ya programu ndogo “A”, asilimia 20 programu ndogo “B”na asilimia 5 kwa programu ndogo “C”. Jedwali la kwanza linaonyesha makisio ya mahitaji ya bajeti kwa miaka mitano ijayo. Jedwali la pili linaonyesha jinsi fedha zinavyoweza kugawanywa katika maeneo mbalimbali ya shughuli.

Makisio ya mahitaji ya fedha ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa miaka mitano ijayo

	TShs (bilioni)	Asilimia ya Jumla
Bajeti ya Maendeleo		
Programu ndogo A – Sekta ya Kilimo na utekelezaji katika ngazi ya Wilaya na ugani	230.2	38
Programu ndogo B – Sekta ya Kilimo ngazi ya Taifa	133.8	22
Programu ndogo C – Masuala yanayoingiliana na sekta nyingine katika ngazi ya taifa	19.2	3
Jumla Ndogo	**383.2**	**64**
Bajeti ya Matumizi ya kawaida		
Mishahara ya watumishi	73.3	12
Matumizi mengine	144.6	24
Jumla Ndogo	**217.9**	**36**
Jumla Kuu	**601.1**	

Kumbuka: Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Idara ya serikali inajumuisha gharama zilizopo. Sehemu ya gharama hizo ni kwa ajili ya mishahara (mishahara ya watumishi) na nyingine ni kusaidia kufanya kazi zilizopo (matumizi mengine).

Makisio yanaongezeka kila mwaka, ina maana, kutoka dola za Marekani milioni 94 kwa mwaka wa 1 hadi dola milioni 54 katika mwaka wa tano.

Jumla ya kiasi kinachotakiwa kimepatikana kwa kuongeza gharama za programu na miradi yote binafsi. Jedwali lifuatalo linaonyesha jinsi fedha zilivyogawiwa mwaka 2002/03. Pia jedwali linaonyesha mapendekezo ya ruwaza za ukuaji ambazo zitahitajika ili kufanikisha ASDP. Haya bado ni makisio yasiyokamilika lakini yanatoa baadhi ya mawazo ya nini kifanyike.

Ruwaza za Shughuli katika Sekta ya kilimo 2002/03 kutoka Serikali ya Tanzania na Wafadhili			**Ukuaji uliopendekezwa**
Eneo la Shughuli	Tsh(milioni)	Asilimia ya Jumla	Asilimia ya ukuaji kwa mwaka
Huduma za ushauri na ugani*	9,404	22	20
Masoko na Fedha*	7,996	19	30
Umwagiliaji	6,919	16	10
Utafiti*	6,527	15	20
Uzalishaji mazao	5,164	12	10
Msaada wa Kitaasisi*	3,749	9	30
Sera na Kazi ya Udhibiti*	1,805	4	40
Uzalishaji wa Mifugo	792	2	10
Uhakika wa Chakula	488	1	10
Asasi za Mafunzo	97	0	10
Jumla	42,941	100	
* = Eneo la Kipaumbele la ASDP			

Kwa muhtasari, Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo unatoa mwongozo wa gharama inayohitajika katika sekta. Aidha mwongozo huu unasaidia katika kuratibu na kutungamana na sera nyinginezo. Vile vile mwongozo huu unaweza kusaidia mambo yafuatayo:-

- Kuelekeza namna rasilimali zinavyofanyiwa tathmini na kugawanya kupitia Utaratibu wa Matumizi wa Muda Mfupi (MTEF) na Tathmini ya Matumizi ya Umma (PER).
- Kuonyesha maeneo yanayofaa kwa wadau wa maendeleo ambayo wanaweza kuchangia.
- Kuhakikisha kuwa vipaumbele katika ngazi ya kitaifa na ile ya chini vinapata raslimali ya fedha inayostahili kutoka serikalini.
- Kuwaeleza wakulima na sekta ya umma kuhusu maeneo ambayo fedha za umma zinaweza kuchangia juhudi zao.



Uendeshaji wa ASDS utaratibiwa na kufuatiliwa namna gani?

Serikali itatoa mazingira mazuri na muundo wa udhibiti kwa maendeleo ya sekta ya kilimo. Haya yataongoza habari za mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ambavyo vitasimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zikifanya kazi kwa ushirikiano na vikundi vya jamii na sekta binafsi katika ngazi ya wilaya.

Idadi kubwa ya wadau itahusishwa katika kuamua jinsi ya kutumia rasilimali, katika kusimamia shughuli, na katika kufuatilia na kutathmini matokeo. Mchoro katika ukurasa unaofuata unaonyesha jinsi kazi itakavyowianishwa na kuratibiwa.

Wawakilishi wa wadau wa ngazi za chini nchini wataungana na wadau wa ngazi ya taifa katika kutoa mawazo katika ngazi ya taifa kwenye Mkutano wa Mwaka wa Wadau. Haya ni mashauriano yanayoongozwa na Rais wa nchi. Mashauriano yanawapa fursa wadau wote kufahamishwa, kujadili na kutoa maoni yao kuhusu maendeleo hivi sasa. Matokeo katika Mkutano wa Mwaka wa Wadau yanatumiwa na Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wakati inapopitia maoni toka ngazi ya juu kuhusu sera, uratibu, kufuatilia na ugawaji wa fedha. Kamati ya Taifa ya uendeshaji inashawishiwa katika njia mbalimbali vikundi vingi vya wadau kama vile Kamati ya Fedha ya Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Kamati ya Ushauri ya Sekta ya Kilimo na Kikundi Maalumu cha Sekta ya Chakula na Kilimo.

Kamati ya Taifa ya Uendeshaji inasaidiwa katika ngazi zake moja kwa moja na Kamati ya Uratibu ndani ya Wizara na Sekretarieti ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) ambayo ina jukumu muhimu katika uratibu na usimamizi wa mchakato mzima. Inayo Mratibu, Ofisa wa Programu, Ofisa wa Fedha na Uendeshaji na wafanyakazi waendeshaji. Inawezekana kuweka wafanyakazi wengine kutegemeana na mahitaji. Shughuli zake ni:

- Kuratibu utekelezaji wa ASDP
- Kurahisisha utafutaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya kilimo
- Kuongeza uhusika wa wadau katika utekelezaji ASDP
- Kurahisisha upangaji bajeti wa ASDP na mchakato wa ugharimiaji
- Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa ASDP
- Kuagiza na kusimamia utafiti unaohusiana na sekta kadri itakavyohitajika

Tanbihi:

Kila Wizara Kiongozi ya Sekta ya Kilimo ina Ofisa Programu wa ASDP ambaye anafanya kazi muda wote katika ASDP na ambaye anashirikiana kwa karibu sana na Sekretarieti ya ASDP.

Zingatia kwamba kuna mifumo ya usimamizi wa ASDP ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja. *Mifumo ya moja kwa moja* inahusisha kazi ya Sekretarieti ya ASDP na ile ya Kamati ya Taifa ya Uendeshaji, Kamati ya Uratibu ndani ya Wizara, Kikundi Maalumu cha Sekta ya Chakula na Kilimo, Kamati ya Ushauri ya Sekta ya Kilimo, na Mkutano wa Mwaka wa Wadau. *Mifumo isiyo ya moja kwa moja* ni ile ambayo inaratibiwa kupitia ASDP lakini inatekelezwa kupitia asasi za umma zilizopo na kupitia mikataba na watoa huduma wa sekta binafsi, vyama vya kitaalamu, wasomi, Asasi zisizo za kiserikali na Asasi nyingine zisizo za umma. Uratibu na usimamizi wa ASDP pia utasaidiwa na wataalamu wa Kikundi Maalumu, Vikundi vya Kazi na Timu za Uundaji kadri itakavyohitajika.

Mchoro wa Uongozi wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo/Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo



Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wa awali ulitokana na ushirikiano, na pia ubora wake hapo baadaye utajengwa katika ushirikiano zaidi - si tu katika mkutano wa mwaka wa wadau bali pia na njia nyingi na ngazi ambapo mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini vinafanyika.

Faharasa: Maana za maneno yaliyotumika katika kitabu hiki

-a utaratibu Iliyopangwa katika mpango au mfumo mzuri.

anuwai Biashara inapokuwa anuwai, inaongeza vitu mbalimbali ilivyonavyo au inavyotengeneza.

asasi Shirika rasmi ambalo linafanya kazi muhimu nchini. Kuanzisha taasisi, pamoja na mambo mengine, kunahusisha kuwa wazi kuhusu kinachopaswa kufanywa wafanyakazi na bajeti vinavyohitajika.

biashara Kununua na kuuza vitu kwa ajili ya kupata faida.

biashara ya bidhaa za kilimo Ni biashara ya upande wa ukulima, inahusisha uzalisahji, usindikaji, usambazaji, na uuzaji wa bidhaa za mashambani.

bidhaa za umma Bidhaa zinazoweza kuzuiwa kutoka kwa mtu mmoja tu kutokana na kuzuiwa kwa wote. Kwa hiyo, wanapaswa kupewa kijumuiya, km. taa za barabarani, ulinzi wa polisi na ulinzi.

demokrasia Ni aina ya mfumo wa kujitawala ambapo watu wanakuwa na sauti katika matumizi ya madaraka mara nyingi kupitia kwa wawakilishi waliochaguliwa, lakini pia kupitia uraghibishi na ushawishi wa vikundi vya wananchi na vyama vya kijamii.

dira Fikra ya jinsi mambo ya baadaye yatakavyokuwa au yanavyopaswa kuwa.

GDP (Pato Ghafi la Ndani) Kipimo cha pato la serikali na shughuli za uchumi. Ni jumla ya thamani ya bidhaa na huduma zote zinazozalishwa kipindi cha muda maalumu (kwa kawaida mwaka mmoja) ukiondoa pato halisi la bidhaa kutoka nje.

hazina Inahusika na mapato ya serikali, hasa kodi.

huduma Hizi ndizo zinazotolewa na sekta za asasi za serikali kuu, mikoa na serikali za mitaa kwa madhumuni ya jamii, siasa, uchumi, biashara na shughuli za biashara. Sekta za huduma zinajumuisha utamaduni na burudani, desturi, elimu, nishati, misitu, afya, sheria, polisi na magereza, ulinzi wa mazingira asili, barabara, usafi, huduma za jamii, utozaji kodi na ukusanyaji mapato, na maji. Kumbuka ubinafsishaji unahusisha kuhamisha majukumu kwa baadhi ya huduma hizi kwenda sekta binafsi.

inayomjali mteja Imebuniwa kukidhi mahitaji ya mteja.

jumuiya Kuna jumuiya zinazoundwa na watu wote wanaoishi katika eneo. Pia zipo jumuiya za maslahi.

kamati Kundi la watu ambao wanapanga mipango au kutoa maamuzi kwa niaba ya asasi.

karabati Kurudishia katika hali ya mwanzo ili kuweza kutumika tena.

kikundi maalumu Kikundi cha watu kilichoteuliwa kutoa ushauri katika utungaji sera au programu. Kikundi kinaweza kukusudiwa kuwa na wadau wengi tofauti ili kishughulike na masuala mtambuko ya sekta na kusaidia kujenga muungano.

kufuata matakwa Huduma (km. ushauri wa kilimo) inafuata matakwa/mahitaji inapowapa watu kile wanachotaka kuliko kile wataalamu wanachofikiria kuwa wanataka.

kujenga uwezo Kuongeza uwezo wa watu, asasi au jumuiya ili kukidhi matakwa yao. Hii ni pamoja na kujenga kujiamini, mafunzo na utoaji wa nyenzo na vifaa.

kulimwa Ardhi ambayo imelimwa kwa ajili ya mazao.

kupewa madaraka Kama kundi la watu litapewa madaraka wanakuwa na udhibiti wa mambo yanayowasibu. Wanakuwa na nguvu na kujiamini zaidi.

kushiriki Katika jamii yenye demokrasia huku kunahusisha ushiriki hai wa watu wa kawaida katika mchakato wa serikali. Kuna viwango vya kushiriki ambavyo vinaanzia katika kupewa taarifa mpaka uhusishwaji kamili na utekelezaji na tathmini ya programu. Kumbuka kuwa sera za ugawaji madaraka na ubinafsishaji zinahusisha haja ya ushirikiki zaidi na mzuri.

kuungana Pale ambapo watu mmoja mmoja wanaungana kuwa kitu kimoja.

kuwa hatarini Kama mtu fulani yuko hatarini, ni dhaifu na ana ulinzi mbaya na anaweza kukabiliwa na shambuio, upinzani na matatizo.

kuwezesha Kurahisisha kufanya jambo. Huku kunaweza kuhusisha kutoa taarifa, kuhamasisha na/au rasilimali za mali vitu, fedha au watu.

lengo Kauli ya wazi ya kitu unachojaribu kufanya. Inasaidia kama malengo ni mahususi, yanapimika, yanakubalika, ya maana na ya muda maalumu.

machinjio Mahali ambapo wanyama wanachinjwa kwa ajili ya kupata nyama.

maendeleo Utaratibu wa kuleta mabadiliko kwa ajili ya maisha mazuri (kupata maendeleo) – kijamii, kiufundi, kimazingira, kiuchumi na kisiasa. Kuna jambo katika kuamua nani afanye au anapaswa kuamua ni kipi kizuri. Ukweli wa nani unatambuliwa?

maendeleo endelevu Hii inafafanuliwa katika Ripoti ya Brundtland mwaka 1986 kama “Maendeleo ambayo yanakidhi mahitaji ya wakati uliopo bila kuafikiana na uwezo wa vizazi vijavyo kufanikisha mahitaji yao”. Hii inaungana na Ajenda ya 21 ya Mkutano wa Rio wa mwaka 1992 ambao ulipendekeza kuwa mipango yote ya maendeleo endelevu ichukue mkabala wa uratibu kukabiliana na masuala ya mazingira, jamii na uchumi.

mageuzi Kufanya mabadiliko katika jambo (km. asasi au utendaji) ili kulifanya liwe zuri.

mageuzi ya muundo Programu ya marekebisho ya soko huria ambayo inawekwa na mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Fedha Duniani kama masharti ya kukopa fedha.

makubaliano ya biashara Mabadilishano ya biashara kati ya watu.

maoni Unapopata maoni kuhusu kitu ulichofanya, unapata mawazo ya uzuri au ubaya wake.

mashauriano Unapoomba ushauri kwa mtu unataka maoni au ushauri. Unapowaomba watu wengi utapata maoni mengi tofauti ambayo yanaweza kujadiliwa.

mazingira Maeneo ambapo mtu au viumbe hai vingine vinaishi na kufanya kazi. Kuna aina nyingi za mazingira (km. asili, jamii, kisheria na uchumi) na yanaweza kuwa mazuri au mabaya. Mazingira yanaweza kuhifadhiwa, kuendelezwa au kuharibiwa.

mazungumzo Majadiliano yenye mtazamo wa pande zote kushinda (shinda/shinda). Haya ni tofauti na mjadala ambapo upande mmoja unashinda na mwingine kushindwa (shinda/shindwa).

miongozo Sheria, taratibu, kanuni na/au ushauri kuhusu jinsi ya kufanya jambo.

miundombinu Vitu vinavyoonekana na vya uendeshaji vinavyohitajika kuendesha biashara au nchi, km. majengo, barabara, umeme na utaratibu wa kujenga na kuitunza.

mjasiriamali Mtu anayeanzisha biashara wakati akijitolea kwa kiasi kikubwa kuthubutu.

mkabala mpana wa sekta Hili ni wazo jipya ambalo linamaanisha mambo tofauti kwa watu tofauti katika mazingira tofauti. Msingi ni kutumia michakato ya ushiriki, wadau wengi kujenga (a) uelewa wa jumla wa matatizo yanayoikabili sekta na kisha (b) mwitiko wa wazi na ulioratibiwa wa matatizo hayo. Wadau mbalimbali wanaona faida kwa kuzingatia umiliki wa serikali, uratibu wa wafadhili, mipango na bajeti ya wazi, taratibu za kawaida za mipango, kuondoa kiasi cha fedha kilichotengwa, kulenga katika utoaji fedha unaozingatia utendaji, ongezeko la busara/mapendekezo katika rasiliamali, na kwa ujumla kurahisisha mchakato wa ugawaji madaraka.

mkabala wa jumla Mkabala unaohusika na sehemu zote za kitu fulani. Programu pana ya sekta ni ya jumla zaidi kuliko mkabala wa mradi.

mkakati Mpango wa muda mrefu ambao unaelezea njia nzuri ya kufanikisha madhumuni maalumu.

mkataba Makubaliano ya kisheria kwa kawaida yanahusika na uuzaji wa kitu au kwa kazi iliyofanywa kwa kiasi fulani cha fedha. Kama ukiingia mkataba na mtu wa kufanya kitu, unaahidi kisheria kufanya hivyo.

mkopo Fedha zinazokopwa ili mtu aweze kununua bidhaa au huduma mapema kwa kuweza kuvilipia moja kwa moja. Watu wanaostahili mkopo ni wale waliolipa madeni yao siku za nyuma.

mkulima mdogo Mtu yeyote anayelima shamba dogo.

mkutano Mkusanyiko rasmi, mara nyingi huchukua siku kadhaa ambapo watu hujali mada.

motisha Kitu kinachohamasisha kufanya jambo. Motisha unaweza kuwa malipo au punguzo kuamsha matokeo au uwekezaji mkubwa.

mpango Mpango wa kina wa jinsi kitu fulani kinavyopaswa kufanya kazi.

mpango (mzunguko) Mipango yenye utaratibu ni mchakato wenye hatua nne:
(1) Chunguza hali iliyopo ili kutambua matatizo na utatuzi unaofaa.
(2) Weka mkakati na mipango ya utekelezaji yenye malengo ya wazi, shabaha na viashirio. Hivi vibainishe nani atafanya nini, mpaka kufikia lini na itagharimu kiasi gani.
(3) Anza kutekeleza mpango na pima viashirio ili kuhakikisha uko katika njia inayostahili.
(4) Chunguza mazingira mapya na kuamua kama mpango au mradi vimefanya kazi kama ilivyotarajiwa na kama kilikuwa kitu kizuri.
Tambua kwamba hatua ya 4 katika mradi wa zamani inaweza kuwa hatua ya 1. Katika mradi mpya na hii inaufanya mchakato kuwa katika mzunguko!

mradi Mpango uliopangwa kwa makini ili kufanikisha malengo yaliyobainishwa wazi katika kipindi cha muda uliopangwa.

mtaala Maudhui ya kozi ya mafunzo.

mtaji Utajiri unaomilikiwa na mtu au asasi. Unaweza kuwekezwa, kukopeshwa au kuazimwa.

muundo Idadi ya sheria au kanuni za msingi ambazo zinaelezea jinsi sehemu za mfumo au wazo zinavyoona.

mwakilishi Mtu ambaye amechaguliwa kuwakilisha au kufanya maamuzi kwa niaba ya mtu mwingine au kikundi.

pambanisha Kusanya na chunguza taarifa.

programu Mlolongo wa matendo, matukio au miradi yenye uhusiano ambayo imepangwa kufikia malengo ya muda mrefu na kufanyika katika kipindi cha muda uliopangwa.

rasilimali Rasilimali za nchi, shirika au mtu ni vitu vinavyopatikana kwa ajili ya matumizi yao, kwa mfano fedha, vifaa na wafanyakazi.

riziki Chochote kinachokupatia kipato chako na kile unachohitaji ili uishi.

sambaza Ambapo jambo (km. taarifa) linapatikana kwa watu wote.

sekta Mgawanyo mdogo wa jamii. Sekta kuu tatu ni (a) sekta ya umma, taifa au serikali, (b) sekta binafsi au ya biashara, na (c) sekta ya wananchi, jamii, hiari/ kujitolea au jumuiya (hii inajumuisha ushirikiano, mashirika ya pande mbili na yanayojisaidia yenyewe). Kumbuka kwamba mara nyingi serikali inachukuliwa kama imegawanyika katika sekta kama Elimu, Afya na Kilimo.

sera	Orodha ya mawazo inatumika kama msingi wa kufanya maamuzi kuhusu kitu gani kinapaswa kuhusishwa katika programu na miradi.
shabaha	Wazo linaloeleweka la kitu unachotaka kufanya (inasaidia kusema ni kiasi gani utafanya na ifikapo tarehe ngapi).
sheria zilizotungwa	(a) Sheria za nchi zinazingatiwa kwa pamoja au (b) mchakato wa kutunga sheria mpya.
shughuli	Hatua ambayo inajaribu kuleta tofauti katika njia ambayo jambo fulani litafanywa.
shughuli (ya biashara)	Biashara au kampuni inayoendeshwa na mawazo thabiti.
shughuli za bajeti	Kukusanya taarifa kuhusu fedha zinazoingia na mahitaji ya matumizi, na kuamua kuhusu njia nzuri ya matumizi.
soko huria	Pale ambapo shughuli za uzalishaji uchumi, usambazaji na ubadilishaji zinafanywa na watu binafsi au biashara kwa kufuata sheria za uzalishaji na mahitaji, na urekebishaji unaofanywa na serikali.
taarifa za soko	Taarifa mpya kuhusu watu na mashirika wananunua na kuuza nini katika ngazi ya chini, taifa na kimataifa. Hii inahitajika ili kuweka mipango mizuri ya biashara.
taratibu	Sheria zinazowekwa na kufuatwa na mamlaka ili kudhibiti shughuli za makampuni na asasi nyingine. Mjadala muhimu wa sera ni kiwango ambacho serikali inapaswa na inaweza kurekebisha shughuli za mashirika ya sekta binafsi-hasa mashirika ya kimataifa.
tathmini	(Angalia ufuatiliaji na tathmini).
tekeleza	Kuufanya mpango uanze kutumiwa.
teknolojia	Matumizi ya maarifa ya kisayansi kwa madhumuni ya vitendo katika ukulima, shughuli, biashara n.k.
toa kipaumbele	Kupanga upya orodha ya vipengele ili vipengele muhimu zaidi na/au vya haraka viwe vya kwanza. Katika mazingira ya wadau wengi inahusisha mashauriano.
ubinafsishaji	Uhawilishaji wa biashara, shughuli au huduma kutoka katika umiliki wa serikali kwenda umiliki binafsi.
uchumi	Uchumi wa nchi au kanda ni mfumo inaotumia kupanga na kusimamia fedha zake, viwanda na biashara au mali ilizopata kutokana na biashara na viwanda [pia angalia soko huria].

uchumi mkubwa Mafunzo/maelezo ya picha nzima ya uchumi, kv. jinsi mali inavyopatikana na kusambazwa. Inaweza kuhusu nchi fulani au kuhusu dunia yote na jinsi nchi moja moja inavyoingia katika sura ya ulimwengu. Mjadala wa uchumi mkubwa unajumuisha:
(1) Tutafanya nini kuhusu matajiri kutajirika zaidi wakati maskini wanakuwa maskini zaidi?
(2) Ni kwa kiasi gani serikali inapaswa kurekebisha "soko huria?
(3) Kwa kuwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira, je ukuaji uchumi usio dhibitiwa unahitajika au unawezekana?

uchumi unaoongozwa Mfumo wa uchumi ambapo nchi inamiliki na kisha kugawa fedha kupitia katika baadhi ya miundo ya mchakato wa mipango mikuu.

ufuatiliaji na tathmini Ufuatiliaji unaohusisha upimaji kadri unavyoendelea ili kuhakikisha kuwa unafuata mpango. Tathmini inahusisha kusitisha mara kwa mara ili kuhakika maendeleo na kuamua kama mpango unahitaji au hauhitaji kubadilishwa. Kumbuka kuwa michakato yote miwili ni rahisi zaidi endapo mpango utahusisha madhumuni na malengo yaliyoelezwa vizuri yenye vigezo na viashirio vilivyowazi.

ugawaji madaraka Kuhamisha mamlaka na majukumu kutoka ngazi kuu kwenda ngazi za chini. Hii inaweza kuwa katika ngazi ya dunia, taifa, wananchi au kaya. Watu wengi wanapohusishwa katika utoaji maamuzi, usimamizi na utoaji huduma katika ngazi zote, kuna uwezekano mkubwa wa maendeleo yanayofaa, endelevu na yenye usawa.

ujenzi wa viwanda Kuongeza kiwango cha shughuli za uchumi ambazo zinahusisha uzalishaji wa mali ghafi na utengenezaji wa bidhaa viwandani.

umaskini Kuna umaskini wa kipato na usio wa kipato. Umaskini wa kipato ni pale ambapo watu wanapata chini ya dola moja ya Marekani kwa siku. Hii ina maana kuwa hawatakuwa na chakula cha kutosha au dawa na watakuwa na mavazi na nyumba duni. Umaskini usio wa kipato ni pale ambapo watu hawana:
(a) haki sawa ya elimu, afya na huduma nyingine za jamii;
(b) heshima na hadhi katika jamii zao;
(c) madaraka na kinachotokea katika maisha yao; na
(d) matumaini ya baadaye.

ushawishi Jambo lililopangwa na wananchi/umma kuwashawishi watoa maamuzi.

ushirikiano/ubia Pale ambapo watu au asasi zinajiunga na wengine kufanikisha lengo na kusaidiana hasara na faida. Ushirikiano unaweza kuwa rasmi zaidi, mkataba au wenye masharti ya kisheria.

ushughulikiaji mambo maalumu Kanuni ambayo Mamlaka Kuu inapaswa kufanya kazi zile tu ambazo haziwezi kufanywa katika ngazi ya chini zaidi.

utatuzi wa matatizo Hatua za sekta ya umma kuwalinda maskini na walio katika shida. Zinaweza kuhusisha mipango ya kazi za umma, hatua za uhakika wa chakula, n.k. Kwa kawaida utatuzi wa matatizo ulifanywa na familia na jumuiya.

utawala Uendeshaji na udhibiti wa kila siku wa shirika au mradi. Utawala unaweza kufikiriwa kama njia ambayo maoni ya viongozi na mameneja yanafanyiwa kazi.

utetezi Kuwa wazi na kuwa na utaratibu kutetea kitu fulani.

utumiaji mashine Hatua ya kutumia mashine kufanya mambo yaliyokuwa yakifanywa kwa mkono.

uwazi Kama sera iko wazi basi ni rahisi kuona inasema nini na hakuna mambo yanayojificha.

uwekezaji Kuweka fedha, muda na/au nguvu katika shughuli ambamo unategemea kupata mapato mazuri.

vyombo vya habari Njia kuu ya mawasiliano ya umma, hasa televisheni, redio na magazeti.

wadau Watu wote wanaopendelea mafanikio ya sera, programu au mradi.

warsha Mkutano ambapo washiriki wanahusika katika majadiliano na shughuli ili kupata matokeo mazuri.

weka mpaka Kama kitu kimewekwa mpaka, maana kikomo/mipaka yake inaonyeshwa wazi ili kukitofautisha na vitu vingine vinavyofanana nacho.

wianisha Kusahihisha au kupanga upya vipengele katika orodha ya mawazo ili yasitofautiane.

wizara kuu Kwa Mkakati wa Kilimo, wizara kuu ni Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ushirika na Masoko, na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Vifupisho

ASDP	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
ASDS	Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
CSO	Vyama vya Kiraia
DADC	Kamati ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya
DADP	Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya
DDP	Programu ya Maendeleo ya Wilaya
FASWOG	Kikundi Maalumu cha Sekta ya Chakula na Kilimo
LGA	Mamlaka ya Serikali za Mitaa
LGRP	Programu ya Marekebisho ya Serikali za Mitaa
MAFS	Wizara ya Kilimo na Chakula
MCM	Wizara ya Ushirika na Masoko
MWLD	Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo
MTEF	Utaratibu wa Matumizi wa Muda Mfupi
NGO	Asasi zisizo za Serikali
PER	Tathmini ya Matumizi ya Umma
PRS	Mkakati wa Kupunguza Umaskini
RDS	Mkakati wa Maendelo Vijijini
SWAP	Mtazamo Mpana wa Kisekta
TDV	Dira ya Maendeleo Tanzania 2025

Kiambatisho cha 1 – ASDP – Programu ndogo tatu

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) inatokana na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS). ASDS ina maeneo ya mkakati 5 yenye matokeo 41 na shughuli 142. Maeneo haya yamepangwa upya ili iwe rahisi kuunda na kuweka bajeti ya mipango ya utekelezaji. Kuna programu ndogo tatu zenye vipengele 10, vipengele vidogo 61 vilivyopendekezwa na uwezekano wa shughuli 111.

Programu ndogo tatu ni:

Msaada na Utekelezaji wa Sekta ya Kilimo katika ngazi ya Wilaya na ugani

Programu ndogo A katika ngazi ya Wilaya itatekelezwa hasa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Inajumuisha shughuli za kusaidia uzalishaji na utengenezaji wa kilimo. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, kazi ya kutoa chakula na huduma utatolewa mkataba kwa makandarasi wa nchini, washauri, asasi za elimu, Asasi zisizo za Serikali na Mashirika ya Kijamii.

Takribani asilimia 75 ya ugharimiaji uliopo utaenda katika programu hii ndogo.

Msaada wa Sekta ya Kilimo katika ngazi ya Taifa

Programu ndogo B katika ngazi ya Taifa inahusisha Mamlaka kuu katika kujenga mazingira mazuri kwa kazi katika ngazi ya Wilaya. Inajumuisha kuihuisha sera, kuboresha muundo wa udhibiti, kusaidia utafiti na huduma za kiufundi na kuhamasisha maendeleo ya sekta binafsi. Ongezeko la kiwango cha kazi hii litatolewa kwa watoa huduma binafsi pale inapobidi.

Takribani asilimia 20 ya ugharimiaji uliopo utaenda katika programu hii ndogo.

Masuala yanayogusa sekta nyingine katika ngazi ya Taifa

Programu ndogo C katika ngazi ya Taifa inahitaji uratibu na ushirikiano mkubwa miongoni mwa idadi kubwa ya wadau. Kazi hii inahimiza muda mwingi na jitihada zaidi lakini si kiwango kikubwa cha uwekezaji.

Takribani asilimia 5 ya ugharimiaji uliopo utaenda katika programu hii ndogo.

Shukrani

Kijitabu hiki kinatoa mwongozo kwa lugha nyepesi na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS). Azma ya Serikali ni kuufanya mkakati huu kuwafikia na kueleweka na watu wengi zaidi.

Uandikaji mwongozo huu ni matokeo ya ushirikiano baina ya wadau mbalimbali. Shukrani za pekee zinatolewa kwa Wizara ya Kilimo na Chakula, Ofisi ya Rais-Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Wadau wa Maendeleo.

Shukrani za pekee zinatolewa kwa watendaji wote wa Sekretarieti ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) kwa kuratibu na kusimamia shughuli za kuandaa mwongozo huu. Pia shukrani hizi za pekee zinatolewa kwa taasisi ya Hakikazi Catalyst iliyotayarisha kijitabu hiki.

Chacha D. Nyakimori
Mratibu – Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)
Februari 2005

Kitabu hiki kimetayarishwa na:
Hakikazi Catalyst

Mchoraji wa Vikaragosi:
Ally Masoud

Usanifu na Uchapaji:
Colour Print (T) Ltd

"Ubora wa maisha unapaswa kupanda kwa kuongeza kiwango cha tija katika sekta zote. Lengo hili linaweza kufanikishwa kwa kubadili uchumi kuwa imara, thabiti na wa ushindani, ukiegemezwa na sayansi na teknolojia.

Mkakati wa kufuata ni ule wa kubadili uchumi kutoka kilimo halisi chenye uzalishaji mdogo hadi uchumi mpana na wenye viwanda wenye sekta mpya vijijini na uzalishaji mkubwa katika kilimo. Hii itazalisha kipato kizuri na kuhakikisha kuwepo na chakula na cha kujitosheleza.

Upanuzi wa uchumi unapaswa kuzingatia programu ya ujenzi wa viwanda inayolenga katika viwanda vya rasilimali za ndani (viwanda vya kilimo) na uwezo wa kukidhi mahitaji ya sekta nyingine wakati ikiendelea kuanzisha shughuli zenye faida - linganishi."

Dira ya Maendeleo Tanzania 2025

Kwa mawasiliano zaidi:

Sekretarieti ya ASDP
Wizara ya Kilimo na Chakula
S. L. P. 9192
Dar es Salaam
Simu: 022-2861344 / 2861346
Barua pepe: asdp.secretariat@cats-net.com